

**TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA OFISI YA KATA YA CHEMCHEM KWA
KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017 WILAYANI RUFJI TAREHE
03.06.2017**

Ndugu Amour Hamad Amour, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2017; Sisi wananchi wa Kata ya Chemchem tunayo furaha kuupokea Mwenge wa Uhuru katika Kata yetu. Tunakukaribisha wewe binafsi pamoja na msafara wako wote unaouongoza katika kufanikisha Mbio za Mwenge wa Uhuru 2017.

Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2014. Mradi huu utakapokamilika utagharimu jumla ya shilingi **40,000,000.00** Kwa kuchangiwa kama ifuatavyo:-

- | | | |
|--------------------------------|--------------|----------------------|
| • Mchango wa Nguvu za wananchi | Tshs. | 3,500,000.00 |
| • Mchango wa Halmashauri (W) | Tshs. | 36,500,000.00 |
| JUMLA | Tshs. | 40,000,000.00 |

Hadi hapa jengo lilipofikia limegharimu Tshs.23, 000,000.00. Kati ya hizo Tshs.4,600,000.00 ni mchango wa wananchi na Tshs.18,400,000.00 ni mchango wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji.

Kata hii inaundwa na vitongoji 7 yenye wakazi **5,133** ambao kati yao wanawake ni **2,687** na wanaume ni **2,446**.

Manufaa ya mradi huu utakapokamilika utawawezesha wakazi wa kata hii kupata huduma za kiutawala kwenye mazingira yaliyoboreshwa ikiwemo maadili na udhibiti wa rushwa.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017, karibu utuwekee jiwē la Msingi mradi wetu wa Ujenzi wa Ofisi ya Kata katika Kitongoji cha Kindwitwi.

“MWENGE OYEE”

MAMLAKA YA MJI MDOGO WA UTETE OYEE!

UTAWALA BORA OYEEEE!

“Shiriki kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Nchi”

SUZAN THOMAS KAWIZA

AFISA MTENDAJI KATA

KATA YA CHEMCHEM